WAZAZI, WATOTO NA C.P.E.

JUMATATU IJAYO, shule za msingi zitafungua milango yake kwa kipindi cha tatu na cha mwisho kwa mwaka huu. Hichi ni kipindi cha mitihani. Ni wakati ama fursa ya wanafunzi kujirekibisha iwapo matokeo yao ya mtihani wa majaribio ya C.P.E. si ya kuridhisha.

Wazee wa Mombasa yataka wende mbio kutafuta matokeo hayo ili watoto wao kimasomo wamefikia wapi. Idara ya elimu ya manispaa ya Mombasa ilifanya jambo la busara kuwatahini wanafunzi wote. Ni msaada kwa walimu, wazee na wanafunzi wenyewe. Siku hizi nafasi za kidato cha kwanza katika shule za Upili hazitolewi kwa rangi, kabila, jina, au dini. Daraja ya kupasi ndiyo inayochagua skuli.

Kuwanunulia watoto mavazi ghali ghali siku za makadara na mwisho wa wiki siyo kumpenda mtoto. Wazazi yataka mara tu shule zikifunguliwa, wahakikishe kwamba watoto wao wanadarisi masomo yao, wanalala mapema na wanajinyima starehe zao zote ili muda wote utumiwe katika masomo. Tusije mwisho wa mwaka tukalia kwa matokeo mabaya ya watoto wetu. Wakati tunao wa kujiandaa. Tuutumieni.

• VIJANA WA Kisilamu ambao walifika State House kumtumbuiza Rais Moi.
PICHA: SAID BURHAN

Mahrus apongeza ziara za Rais Moi Pwani

ZIARA ya Rais Moi Pwani imetia nuru mambo mengi ya umoja, upendo na amani alisema mwenyekiti wa Baraza la Lamu, Diwani Ali Mahrus ambaye pia ni mwenyekiti wa Kanu Wilayani Lamu.

Akiongea na shirika la habari la Kenya Diwani Mahrus alisema "Upendo wa Rais Moi kwa wananchi wake umedhihirika kila sehemu ya Pwani, na ni hatua ambayo itadumisha maisha mema Kenya". Alisema "Niliwongoza ujumbe wa Lamu wa Kisilamu kumlaki Mtukufu Rais Moi huko State House Mombasa, na tulifurahi sana kukutana naye tena uso kwa uso na kufahamiana naye kwa mengi".

Bw. Mahrus alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Pwani Bwana Luka Galgalo kwa bidii na utumishi wake halisi kwa wananchi wote wa Pwani.

Kwa niaba ya ujumbe wa Lamu Bw. Mahrus alithibitisha imani kamili kwa Mtukufu Rais Moi, serikali na chama kinachotawala cha Kanu.

MKUTANO WA waandishi wa magazeti ya mashambani ulifanywa Nairobi hivi majuzi. Hapa mhariri wa gazeti la Wizara ya Habari na Utangazaji Sauti ya Kwale Bw. Faraj Dumila anaonekana katika mkutano huo ambao pia aliuhutubia. Upande wake wa kushoto ni Bw. Abel Ndumba, Afisa wa Uandishi na Mtafiti Wizara ya Habari na Utangazaji Kenya.

SAUTI YA KWALE

WAZIRI wa Habari na Utangazaji Bwana Aringo alitangaza kubuniwa kwa gazeti la mashambani Wilayani Kwale ambalo litasimamiwa na Mhariri Bwana Faraj Dumila.

Akihutubia mkutano wa viongozi na wakuu kadha huko mjini Kwale Waziri huyo wa Habari na utangazaji alisema "ni lengo la serikali kuwatumikia wananchi wote na kuwafahamisha wajibu wao kwa taifa lao kwa utumishi unaofaa, na wao kuwa timamu kwa mafunzo na mwongozo waserikali yao".

Waziri aliandamana na manaibu wa mawaziri wake Bwana Nteere Mbogori, Bw. Alphonse Okuku, na Mkurugenzi wa Habari nchini Kenya Bwana Laban Kabiru, Katibu wa kudumu wake Bw. John Gituma pamoja na Mkuu wa Habari Mkoani Bwana Walter Nyawanda.

Aliwataka wananchi wa Kwale kulipokea gazeti hilo lao kama chombo cha maendeleo, gazeti hilo *Sauti ya Kwale* litaleta maendeleo Kwale.

Propaganda Mbovu za Nchi Jirani: Akihutubia mkutano wa wakuu na Viongozi huko Kilifi mjini Waziri wa Habari na utangazaji Bwana Peter Aloo Aringo alisema Kenya inadumisha msingi wake wa ujirani mwema lakini sivyo kamwe inavyofanywa na mataifa jirani ambayo kila mara hutupia Kenya maneno mabaya na ya uchochezi usio msingi.

Alisema serikali inafahamikiwa yote na kwamba ni lengo la Sauti ya Kenya kupanuliwa ili kutoa utumishi mzuri.

Baraza la Mombasa kupata idhini upya kwa mipango

na KENYA NEWS AGENCY

BARAZA la Mombasa limeshauriwa na Waziri wa Serikali za Wilaya Bwana Stanley Oloitiptip kupata kibali upya cha mipango yao ya maendeleo ambayo haikutekelezwa katika miaka iliyopita.

Akihutubia baraza la mji wa Mombasa Bwana Oloitiptip katika risala yake kwa baraza la Mombasa alifahamisha na kusema "kila mpango ulioahirishwa kutekelezwa ni lazima kupawa kibali chake upya hasa kwa vile fedha zinazohitajika ni nyingi mno".

Kati ya mipango aliyoitaja ni upanuzi wa soko la jumla la Muembe Tayari. Mipango ya makao ya Likoni na Kisauni, mipango ya kupata ardhi zaidi kwa maendelo na kadhalika.

Mapato ya baraza mwaka uliopita yalikuwa jumla ya pauni 4,553,460 na mwaka huu mapato yamekisiwa kufikia pauni 5,041,565 na yameidhinishwa na Waziri. Nyongeza imefika kipimo cha pauni 488,105.

Idhini nyingine ni ya kuruhusu kutolewa kwa kazi zilizokuwa hazipata watumishi na kufikiriwa mipango mipya ya kutoa kazi.

SAUTI YA MVITA IRIJESHWE PWANI KUPAMBANA NA UCHOCHEZI JIRANI

KENYA NI taifa huru, taifa moja, taifa lenye msingi wa amani, umoja na maendeleo. Ni taifa bora zaidi katika Afrika Mashariki tukitaka tusitake. Bila ya shaka sifa ya Kenya. Umoja wa Kenya, upendo wa Kenya, maongozi ya Kenya, yote haya yanakabiliwa na uhasidi unaozidi kila siku. Twasikia kwa masikio yetu jinsi uhasidi unavyozidi kutendewa Kenya kila siku na mataifa jirani. Na zaidi kwa kupitia katika Vipindi vya Radio ambazo kila mara hufuata mbinu za kitamaduni ili kujaribu kuwapotosha wananchi wa Pwani ya Kenya, wananchi wa Kaskazini Mashariki ya Kenya, na sehemu kadha za Kenya.

Waswahili wasema kinolewacho hupata, na kupata huku si lazima kuwe kupata kunaweza kunyoa ndefu au masharubu, lakini hata kupata na kuweza kujaribu tu. Huo ndio mwisho na lengo la Uhasidi.

Waziri hodari mwenye bidii, Waziri wa Habari na Utangazaji nchini Kenya Mheshimiwa Bw. Peter Aloo Aringo alisema hivi majuzi mjini Mombasa kwamba "Kenya yafahamu vizuri visa vya maneno maovu yanayolengwa nchini kila siku kutoka nchi jirani". Pwani ya Kenya Mheshimiwa Bwana Waziri wa Habari na Utangazaji kulikwa na chombo kamili cha kupambana na uovu kama huo. Chombo hicho kilikuwa Sauti ya Mvita.

Stesheni Radio Shupavu ambayo mataifa yote jirani yalikuwa hayawezi kuvuta pumzi wakati ikinguruma. Leo ni silaha hiyo hiyo ambayo irudishwe papa hapa Pwani ili ndugu zetu katika Sauti House waweze kuvurumisha vipindi vya kitamaduni na maendeleo Pwani ili kupambana na vitendo hivyo vya mataifa jirani. Silaha hiyo tu ya Sauti ya Mvita ndiyo ya pekee itakayozidi kudumisha maongozi ya mpendwa Mtukufu Rais Moi, serikali yetu, chama chetu cha Kanu na maendeleo ya watu wetu. Wanaokwambia kuwa ipo njia nyingine, hao nao pia si wa kuaminiwa. Na majuto ni mjukuu.

SHEREHE ZA kuadhimisha mwaka wa mia moja tangu kujengwa kwa msikiti wa Memon Nasserpuria Jamia Mosque zitafanywa siku ya Jumaamosi tarehe 20/9/80 wala si kesho. Ummati mkubwa unatarajiwa kuhudhuria sherehe hizo zitakazoanza saa kumi na nusu jioni. Picha yetu inaonesha sehemu ya msikiti huo uliojengwa mwaka 1880.

NDIMI MWANA MASIKINI

Naamka asubuhi,
Kinywaji wala siwahi
Kwani kitanabahi
Yatima, kilema mimi

Ninazo nguvu hakika
Si kwa kuwa nilitaka
Maisha ya kusumbuka
Yatima, kilema mimi

Siku nilipozaliwa
Nilipo anza kukaa
Hivyo nililelewa
Yatima, kilema mimi

Hawo walionilea
Mzigo wakautua
Udhia kunifanyia
Yatima, kilema mimi

Ikabidi kutoroka
Kaanza kutaabika
Kweli jua likawaka
Yatima, kilema mimi

Ulimwengu kanifunza
Mwenyewe nikajitunza
Kila kazi kaifanza
Yatima, kilema mimi

Sasa hebu nambieni
Mwanitia masimangoni
Dhiki yangu jamani
Yatima, kilema mimi

Wewe unayo bahati
Huwezi kulizatiti
Mimi mtu wa tiati
Yatima, kilema mimi

Mimi sikuombi kitu
Kitaka nifanyia utu
Siku lazimishi katu
Yatima, kilema mimi

Ukitaka kunipata
Kila njiani kipita
Riziki nikitafuta
Yatima, kilema mimi

Nyumba za mayatima
Pia zile za vilema
Kitaka msaada tuma
Yatima, kilema mimi

Chochote takacho toa
Ujahili utauvua
Madhambi utayatua
Yatima, kilema mimi

Jua bado liko chini
Kukitia kanwani
Sina kitu nyumbani
Ndimi mwana masikini

Lakini sina elimu
Dunia linidhulumu
Kwangu mimi yalidumu
Ndimi mwana masikini

Mamangu alifariki
Baba pia hakubaki
Na majirani rafiki
Ndimi mwana masikini

Nyoyoni ikesha hamu
Wakaninyima elimu
Pia kunishitumu
Ndimi mwanamasikini

Kwa kutofuta maisha
Dhiki isiyokwisha
Pasi na mvua kunyesha
Ndimi mwana masikini

Mengi nisiyo yajua
Kwa nguvu kuzitumia
Pasipo kuzichagua
Ndimi mwana masikini

Haya ni makosa yangu
Na aloninyima Mungu
Ya jadi tangu na tangu
Ndimi mwana masikini

Ya kuzaliwa tajiri
Tatizo la ufakiri
Wanifanyia Kiburi
Ndimi mwana masikini

Mwenyewe unayo macho
Kinipa cho chote ndicho
Sije kanipa kisicho
Ndimi mwana masikini

Huwezi kunikosa
Taona nikipapasa
Bila macho huikoso
Ndimi mwana masikini

Ndiyo yangu maskani
Ndipo hasa nyumbani
Au ulete mkononi
Ndimi mwana masikini

Hakita kataliwa
Na kupata majaliwa
Kwa Mungu utaridhiwa
Ndimi mwana masikini

na SAID ABDULLA OMAR, P.O. Box 81261, MOMBASA.

Coastweek ★★

SWAHILI CROSSWORD NO. 94

KWENDA KULIA:

1. Ni guu lakini si la kiumbe mwenye uhai
5. Umbo la mtu lilivyo
7. Anayepasha tohara
9. Inadi, kero
12. Mahali pa kupashwa tohara
13. Tenza nguvu
15. Namna ya mnyama wa mwitu
16. La mlua, boma
17. Namna ya
20. Katikati ya chombo kama jahazi

KWENDA CHINI:

2. Tizama, angalia
3. Kivuko
4. Huwa juu ya wali
6. Ona usingizi
8. Aina ya boga
10. Mdomo mkubwa
11. Huwa kati ya milima miwili
14. Namna ya tunda
18. Hapana, sitaki
19. Funga ndoa

UNGA SAFI NO. 1
WA MAHINDI



JINA........

SANDUKU LA POSTA

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 92:

[1] Haji A. Barawa, Sanduku la Posta 54, Mariakani,

[2] Habibu Omari, Sanduku la Posta 81211, Mombasa,

[3] Shamim Zein, Sanduku la Posta 90190, Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 92 —

KWENDA KULIA:

1. MKWEZI, 5. IKULU, 7. UNGAMA, 8. BELUA, 11. ZAGAA, 12. INA, 15. MWANYA, 17. KUUMENI, 18. GK.

KWENDA CHINI:

1. MHUNZI, 2. WAGOGO, 3. ZIMBABWE, 4. IKAE, 6. LAU, 9. LAINI, 10. APAA, 13. NY, 14. FUO, 15. MMA, 16. ANA

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindo watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa 'T'-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na ATTA LTD, Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Alhamisi tarehe 11.9.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.